# CLASS 8 HOLIDAY HOMEWORK TERM 2 2020

# KISWAHILI

## KUZIKILIZA NA KUZUNGUMZA

1. Kamilisha Methali: Ivumayo ______________ 1.
   A. haimudu
   B. haidumu
   C. ni mbovu
   D. hurumisha
2. Kati ya maneno haya, lipi si la adabu? 2.
   A. Samahani
   B. Nipatie
   C. Tafadhali
   D. Naomba
3. Jibu la "***Makiwa***" ni ______________ 3.
   A. Asante au nashukuru
   B. Ni hayo au ni makubwa
   C. Tunayo au yamepita
   D. Tupo au tumepaoa
4. Shairi la majadiliano kati ya watu wawili au zaidi ni ______________ 4.
   A. Tathlitha
   B. Tamthilia
   C. Utenzi
   D. Ngonjera
5. Tegua kitendawili: Chali mwembamba anampiga chali mnene 5.
   A. Shoka
   B. Mkwiro
   C. Mchi
   D. Fimbo
6. Msemo au nahau "***Kula ngwamba***" una maana gani? 6.
   A. Kulima kwa nguvu
   B. Kufanya kazi ngumu
   C. Kula kwa pupa
   D. Kutoka bila mafanikio
7. Methali "***Kipendacho moyo ni dawa***" ni sawa na ______________ 7.
   A. Adui mpende
   B. Moyo ni pango la maneno
   C. Kipenda roho hula nyama mbichi
   D. Cha moyoni kisitiri
8. Kamilisha tashbihi: ***Yeye ni mnyamavu kama*** ______________ 8.
   A. bubu
   B. kaburi
   C. maiti
   D. kondoo
9. Wanawake wanapoitwa huitika ______________ 9.
   A. Naam!
   B. Beka!
   C. Aisee!
   D. Eeh!
10. Tulipokuwa tukiogelea bwawani tulipiga kachombe ______________ 10.
    A. tang!
    B. pu!
    C. tifu!
    D. chubwi!
11. Makanga anadaiwa madeni mengi. Kwa hivyo anadaiwa ______________ 11.
    A. kope si zake
    B. pata potea
    C. hapa na pale
    D. maskini hohehohe

12. Ng'ombe aliponea chupuchupu. Maana yake ni ________
A. alipona
B. alinusurika
C. alitoroka
D. aliumia

13. Ni jibu lipi ambalo si sehemu ya shairi?
A. Utao
B. Mkarara
C. Inksari
D. Tathnia

14. ***"Siku za mwambo"*** maana ya nahau hii ni siku za ________
A. furaha
B. huzuni
C. shida
D. za mambo mengi

15. Kupiga chafya ni kuchemua: ***Kupiga mbweu ni*** ________
A. kugeuka
B. kuteguka
C. kuteuka
D. kubiruka

16. Neno "***shukrani***" lina silabi ngapi?
A. Tano
B. Tatu
C. Nne
D. Nane

17. Mtu akiwasalima "***Mpo***?" Mtamjibu
A. Tuko!
B. Tumo!
C. Ndiyo!
D. Tupo!

18. Sentensi hii imetumia fani gani ya lugha?
***Makau ni sungura, anakudanganya.***
A. Tanakali
B. Tashbihi
C. Istiara
D. Nahau

19. Mwanajeshi hatikisiki, yeye ni imara kama ________
A. simba
B. mwamba
C. nanga
D. ndovu

20. Kamilisha kitendawili kifuatacho
***Tandika mkeka tule kunazi***
A. Kitanda
B. Jua
C. Mlo
D. Nyota

21. Mkono mzuri ni kwa fanaka kama ilivyo ________ kwa kuondoa kiu ya maji
A. piga chafya
B. kunga roho
C. piga maji
D. kufa ganzi

22. Ni kundi lipi lenye irabu pekee?
A. a,b,ch,dh
B. baba, kaka, dada, lala
C. ba, fa, ma, tha,nya
D. a,e,i,o,u

23. Tumia vitate mwafaka kujaza mapengo; Moto huyu hawezi ________ akiwa na nidhamu kutokana na ________ yake.
(Kukuwa, kukua, Mazingira, mazingara)

| |
|---|
| 12. |
| 13. |
| 14. |
| 15. |
| 16. |
| 17. |
| 18. |
| 19. |
| 20. |
| 21. |
| 22. |
| 23. |

| | |
|---|---|
| **24.** Tumia takriri mwafaka kujaza pengo<br>Mgonjwa huyo hajui_______________yu katika pumzi zake za mwisho<br>A. aingiaye wala atokaye<br>B. hana hanani<br>C. la mwadhini wala la mteka maja msikitini<br>D. kutia na kutoa | **24.** |
| **25.** ***Tumia jibu mwafaka***<br>Baba watu aliwaonya kuhusu hatari ya kuwa na inda na inadi maishini kama ___________________<br>A. mtu na kivuli chake<br>B. maji na mafuta<br>C. ulimi na mate<br>D. joka la mdimu | **25.** |

## KUSOMA

## UFAHAMU 1

***Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali***

Kuna aina nyingi za sanaa. Mashairi ni mojawapo ya sanaa kubwa yenye maana fiche. Mashairi huwa tungo zenye lugha nzuri iliyojaa utamu wa matamshi. Lugha ya Kiswahili hutumia maneno machache. Maneno haya huhifadhi maana iliyokusudiwa na mshairi.

Zipo aina mbalimbali za mashairi kama vile tathnia, tathmina, tathlitha, tarbia, takmisa na kadhalika. Aina hizi huitwa bahari. Wingi au uchache wa beti hutegemea uzito wa mawazo ya shairi, yanayoelezwa na mshairi. Kwenye ubeti hupatikana mishororo inayofuata mizani maalum kulingana na aina ya shairi. Aghalabu, aina ya tarbia hutumiwa na washairi wengi zaidi ya tathlitha na takhmisa. Aina ya tarbia huwa na mizani kumi na sita katika kila mshororo. Mshairi ni mtu aliye na kipawa cha kutunga mashairi.

Malenga ni mtu anayejua kwa mapana na marefu lugha na ni bingwa wa sanaa hii. Msanii anapoeleza jambo hutumia lugha kwa njia ya kipekee. Wakati mwingine mshairi hufupisha au kurefusha maneno akilenga mtiririko wa mizani na vina bila matatizo. Kwa hivyo si ajabu kwamba mshairi huikuza na kuitukuza lugha kwenye tungo zake. Vilevile washairi huonyesha uzalendo kwa kuisifu nchi na viongozi wao katika mashairi yao. Aidha mshairi anaweza kuwashawishi wasikilizaji au wasomaji watende au wasitende jambo fulani. Kupitia kwenye mashairi tunaweza kuelimika si haba. Hivyo basi ni bora tukubali na kuyaenzi mashairi na hata ikiwezekana tujitose kwenye ulingo huu wa utungaji, uimbaji na kukariri mashairi.

1. Kisawe cha kipaji ni ______________________
   A. usanaa
   B. taji
   C. paji
   D. kipawa
   1.
2. Ni kitu gani kisicho budi katika ushairi?
   A. Uwezo wa lugha
   B. Utumiaji wa lugha mufti
   C. Kipawa cha kipekee
   D. Aina za bahari za ushairi
   2.
3. Ni maneno gani yaliyotumiwa katika taarifa na yana maana ya maneno machache?
   A. Maneno haba
   B. Maneno yenye maana iliyofichika
   C. Maneno ya mshairi
   D. Maneno makubwa
   3.
4. Mshairi huitwa bingwa kwa kuwa ______________________
   A. yeye hutunga mashairi
   B. yeye amelisoma vitabu vingi
   C. yeye ana ujuzi na kipawa cha utungaji mashairi
   D. yeye hufupisha na kurefusha maneno
   4.
5. Shairi la Kiswahili hugawanyika katika ______________________
   A. uzuri wa lugha
   B. paragrafu mbalimbali
   C. wingi na uchache wa maneno
   D. vifungu au beti
   5.
6. Mishororo yenye mizani kumi na sita hupatikana kwenye shairi la?
   A. Tathlitha
   B. Takhmisa
   C. Tarbia
   D. Tasdija
   6.
7. Maana fiche ni sawa na ______________________
   A. Maana ya juu
   B. Maana iliyofichamana
   C. Maana iliyofichua
   D. Maana ya malenga
   7.
8. Mashairi si ______________________
   A. tungo zenye utamu wa maneno
   B. tungo zenye utamu wa kucheza
   C. tungo zenye utamu wa mtiririko
   D. tungo zenye utamu wa kukariri
   8.
9. Kulingana na taarifa, mshairi haonyeshi uzalendo wake kwa ________
   A. kutunga mashairi ya kusifu nchi na viongozi wake
   B. kutumia lugha yenye hadhi ya juu
   C. kutunga mashairi ya adabu na kuelimisha
   D. kuwakashifu viongozi pasipo na haja ya kufanya hivyo
   9.
10. Maudhui ya taarif hii ni ______________________
    A. Mshairi na tungo za uzalendo
    B. Mshairi na mwenye utamu na matamshi
    C. Mshairi na aina za mashairi
    D. Mshairi na tungo za uzalendo
    10.

## UFAHAMU 2

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali***

Tofauti na baadhi ya wasanii hasa wanaochipuka, ambao hujihusisha na fani hii kujifurahisha, kwa msanii huyu muziki ni taaluma na kitega uchumi.

"Ninafanya kazi hii kama njia ya kujipatia riziki kwani hadi sasa ninategemea muziki kujikimu kimaisha. Mimi hupata pesa ninapoalikwa kufanya maonyesho kuanzia elfu hamsini na zaidi kulingana na mipangilio ya sehemu nilioalikwa," akaelezea.

Aliendelea kusema muziki humwezesha kuimarisha lugha ya Kiswahili, ufanisi uliompelekea kutambuliwa katika tuzo hizo za Kiswahili. Kando na wasanii wengine chipukizi ambao hukiri kupata pingamizi ya kuendelea na muziki kutoka kwa wazazi wao, Amina Zara hakukumbana na hayo.

"Jamaa zangu na hasa wazazi walikubaliana na uamuzi wangu wa kuwa mwana muziki kwa sababu walitambua uwezo wangu. Kutokana na hilo hawakuwa wa budi ila kuniunga mkono huku wakinitakia ufanisi mkubwa," alisema.

Lakini hii haimaanishi mwanamuziki huyu huyu hana changamoto kama wasanii wengine wanaojaribu bahati yao katika fani hii.

"Mojawapo ya shida ambazo nakabiliana nazo ni kukosa meneja au promota wa kuniendeshea shughuli zangu za kimuziki. Hili limekuwa tatizo kwani ni watu hawa ambao huwa na jukumu la kuwashauri wasanii kuhusu sekta hii," alieleza.

Aidha, asema sekta ya muziki siku hizi imeingiwa na ufisadi ambapo nyimbo za msanii haziwezi kuchezwa bila kujuana au kulipa hela.

**1.** Neno "chipuka" limetumiwa kumaanisha ______________________ **1.**

A. mmea mdogo
B. wanamuziki
C. wasanii wadogo
D. uchumi na biashara

**2.** Ipi si njia bora ya kujipatia riziki? **2.**

A. Kuwa dereva
B. Kuwa hawara
C. Kuwa utingo
D. Kuwa kandawala

**3.** Mwandishi hupata pesa wakati gani? **3.**

A. Anapozurura kama mbwakoko
B. Anapotumbuiza hadharani
C. Anapoziokota pesa
D. Anapoalikwa kufanya maonyesho

**4.** Ni gani kati ya haya chipukizi huyu hakupata kutokana na muziki?

A. Uzembe
B. Kuenzi Kiswahili
C. Ufanisi
D. Kupata darahimu

5. Chipukizi huyu alipata kutiwa moyo na nani ili aendelee katika Nyanja ya muziki?
   A. Jamaa zake
   B. Babu yake
   C. Jirani zake
   D. Jamii yake

6. Maneno "***kuunga mkono***" ni aina ya ______________
   A. methali
   B. tanakali
   C. nahau
   D. wimbo

7. Mojawapo ya changamoto ambazo chipukizi huyu anapata ni ________
   A. kukosa wazazi wazuri
   B. kupata pesa nyingi
   C. kukosa meneja
   D. kupata promota

8. Kazi kuu ya maneja ni ______________
   A. kushauri na kuendesha shughuli
   B. kupata mshahara mkubwa
   C. kutumia mali vibaya
   D. kuzembea kazini

9. Neno ufisadi limetumiwa katika taarifa linamaanisha?
   A. Malipo mengi
   B. Malipo yanayofaa
   C. Malipo makubwa
   D. Malipo yasiyofaa

10. Taarifa hii inahimiza vijana?
   A. Kuupa uzembe kipau mbele
   B. Kutojikimu maishani
   C. Kuwa na bidii
   D. Kulaza damu

| |
|---|
| |
| 5. |
| |
| 6. |
| |
| 7. |
| |
| 8. |
| |
| 9. |
| |
| 10. |
| |

## UFAHAMU 3

Nilichaguliwa kuwa kiranja mkuu wa shule ya maghulamu ya Butula mbele ya umati mkubwa. Uchaguzi huu ulikuwa kwa njia ya kura ya wazi. Majina ya wote waliopendekezwa kugombea uongozi yalisomwa. Tulipiga foleni uwanjani, kisha wanafunzi wakaruhusiwa kusimama nyuma ya yule waliyempenda kuwa kiranja wao mkuu.

Mlolongo wa vijana waliokimbilia nyuma yangu kuniunga mkono haukufananishwa na wa wengine. Nilimshinda mpinzani wangu wa karibu mbele ya walimu, wanakamati na hata washikadau wote wa kijiji chote cha Butula kwa kiwango kikubwa. Papo hapo nikagundua kuwa kumbe nilikuwa mtu wa watu. Naam! Chanda chema... na mcheza kwao hutuzwa. Mwalimu wetu mkuu, Bwana Ali hakuficha furaha yake nyingi alipokuwa akilitangaza jina langu waziwazi na hadharani.

Nilifanya kazi yangu ya kiranja mkuu <u>barabara</u>. Hili halikunizuia kutia fora masomoni. Nililaani kushika mkia katika mtihani wowote shuleni. Hata hivyo, maendeleo haya mazuri yalichafuliwa na mfanyi kazi mgeni, bwana Hassan kwa kunisingizia kuwa na mkono mrefu. Nitamlaani milele kwa wazo hilo.

Nilihurumiwa pakubwa na vijana wenzangu, walimu, wazazi na washikadau wengine. Kweli dua la kuku halimpati mwewe.

1. Msemaji alikuwa wa jinsia ipi?
   A. Kiume
   B. Kijana
   C. Kike
   D. Huntha
2. Uchaguzi huu ulikuwa wa kidemokrasia kwa njia ya ______________
   A. siri
   B. faragha
   C. turufu
   D. mlolongo
3. Msimulizi wa makala haya alikuwaje kimasomo?
   A. Zuzu
   B. Wembe
   C. Bwege
   D. Mzembe
4. Ni mabadiliko yapi yaliyomkumba msimulizi baada ya uchaguzi?
   A. Kuhurumiwa na vijana
   B. Kuchaguliwa kuwa kiranja mkuu
   C. Kuletewa mfanyikazi mgeni aliyemhurumia
   D. Kupachikwa kwa yeye ni mwizi
5. Msemaji kuhurumiwa na wenziwe kulionyesha?
   A. Alihurumiwa
   B. Alipendwa
   C. Alionewa
   D. Aliumizwa
6. Kamilisha methali hii. Chanda chema ______________
   A. ni kizuri
   B. hakikosi pete
   C. huvikwa pete
   D. ni cha shahada
7. Toa tarakimu kamili ya nomino mahususi ya watu yaliyotajwa
   A. Manne
   B. Matano
   C. Mawili
   D. Mengi
8. Neno "***barabara***" limepigiliwa mstari kumaanisha
   A. Vizuri
   B. Waziwazi
   C. Njia kubwa
   D. Si pwani
9. Ni tamathali ipi ya lugha iliyotumiwa na msemaji mwisho wa makala haya?
   A. Tashbihi
   B. Nahau
   C. Kitendawili
   D. Methali
10. Ni nini kichwa mwafaka cha makala haya
    A. Uaminifu
    B. Mwalimu
    C. Uchaguzi shuleni
    D. Hadithi

| |
|---|
| 1. |
| 2. |
| 3. |
| 4. |
| 5. |
| 6. |
| 7. |
| 8. |
| 9. |
| 10. |

## UFAHAMU 4

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***

Simu yangu ilikuwa imeisha chaji kwa muda wa saa tatu. Kwa muda huo wote sielewi ni wangapi walionitafuta wakanifutu. Bila shaka waliniita mteja, lakini mimi, ninaamini kwamba ningekuwa mteja ningewahudumia nao

wangenihudumia. Huo ndio uhusiano kati ya mhudumu na mteja. Lakini haya tuache. Turejee tezi ili tushike omo tutokee ngamani.

Nilichaji rununu hiyo na kurejelea kazi yake, ndipo nikasikia ikikiriza kwa kani. Nilibofya kipokezi na kuipachika sikioni. Nikasema, "aisee!" Nilipoitikiwa, nilitambua kuwa sauti ilikuwa ya uchanga kutoka kwa mtu mchanga. Alinivaa kwa mawali mfululizo kuhusu maneno ya Kiswahili. "Nini maana ya maneno yafuatayo: Sinza, fuiya, kituitui, adha, gatuzi, fyuka na mwisho, neno maiti liko katika ngeli gani?"

Mimi hupenda kuyajibu maswali ya kila mtu kupitia mawasiliano ya rununu. Kuuliza si ujinga. Lakini kama huku ndiko kupigiwa simu na kuvamiwa kwa mawali bila hata salamu, basi ada ni adha. Tena ni adha inayokaribiana na adhabu hasa. Pili, mbona mtu asijitambulishe? Kusema mimi ni Fulani wa Fulani, wa mahali Fulani, naomba kuuliza swali, kuna ushuru gani? Kuna ushuruti wowote?

Tatu na zito zaidi ni kwamba, kwa nini mtu aulize mtiririko wa maneno ambavyo yanapatikana moja kwa moja katika kamusi pamoja na ngeli na maelezo yake? Tukiwajibika tutaelimika kwa kujielimisha zaidi kuliko mauzauza ya kuulizauliza japo mambo yanapatikana ndani ya mikoba yetu ya vitabu.

1. "Simu ilipoisha chaji" maana yake ni kuwa ____________
   A. Ilikufa
   B. Iliisha kawi
   C. Ilizimika
   D. Ilipotea
2. Mtu akikutafuta kwa simu kasha asikupate tunasema ____________
   A. amekufutu
   B. amekufuta
   C. amekukosa
   D. amekuhepa
3. Mteja ni mtu ____________
   A. anayekwenda kupata huduma
   B. anayekosekana kwenye simu yake
   C. anayetafutwa kwa simu
   D. anayezima simu
4. Simu ilipokiriza, msemaji alifanya nini?
   A. Aliudhika
   B. Aliibofya
   C. Aliijibu
   D. Aliuliza swali
5. Mtu aliyempigia msemaji simu
   A. alimakinika
   B. alituama
   C. alipaparika
   D. disihi.
6. Mpiga simu alikosa umakini gani?
   A. Kujitambulisha na salamu
   B. Kuuliza kwa Kiswahili
   C. Kutuma rununu vizuri
   D. Kutumia kamusi

| |
|---|
| 1. |
| 2. |
| 3. |
| 4. |
| 5. |
| 6. |

7. Msimulizi anaposema "turejee tezi ili tushike omo" anamaanisha nini?
   A. Twende mbele kisha turudi nyuma
   B. Tunyamazie hapo
   C. Turudi nyuma kisha tusonge mbele
   D. Tuingie melini
8. Kuuliza maneno yanayopatikana waziwazi kwenye kamusi kunadhihirisha nini?
   A. Watu hawana kamusi
   B. Watu hawajui kutumia kamusi
   C. Wengi wetu ni wasumbufu
   D. Kuhepa wajibu wa kujituma
9. Mlahaka mwema uliokiukwa katika habari hii ni?
   A. Kujitambulisha, salamu na kutafadhalisha
   B. Kupiga simu kwa sauti ya juu
   C. Kuuliza maswali mengi
   D. Kumtafuta mwenye simu sana
10. Mauzauza ya kuuliza maswali yana athari gani?
   A. Huongeza wajibu wa kujifanyia utafiti
   B. Humnyima mtu uwezo wa kutumia kamusi kikamilifu
   C. Ni njia ya mkato ya kujifunza
   D. Kupata majibu ya haraka

| |
|---|
| 7. |
| 8. |
| 9. |
| 10. |

## KUANDIKA

***Mtungo 1: Jaza mapengo***

____1___ uzuri wa ___2___ ndani ni kipande cha mti. ___3___ kijiji cha Tafuta waliishi wanawake wawili, Zipu na Pata. Walipendana na ____4___ kwa lolote na chochote walichotenda. ___5____walikuwa kama ___6____. Urembo wao ___7___ na ule wa hurulaini. Urafiki wao ____8___ ni urafiki wa kiwango ___9___. ____10___ zipu alianza kumwonea gere Pata, kwa kuwa maisha yake ___11____ faraja na starehe za Sultani bin Jerere. Maisha ya ___12___ yake pia yalianza kwenda ndivyo sivyo. Aliamua kwenda kwa mganga kutafuta suluhisho. ___13___ rafiki __14____ Pata aandamane naye, ila alisusia. Mganga alipomwona alifurahi kwani alijua angepata ____15____.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. Kama | B. Kwani | C. Aidha | D. Angalau |
| 2. | A. kuyu | B. mkakasi | C. mkaasi | D. mabuu |
| 3. | A. Kwa | B. Kwenye | C. Katikati | D. Katika |
| 4. | A. kufaana | B. kufanana | C. kuonana | D. kusaidiwa |
| 5. | A. Yamkini | B. Lakini | C. Yakini | D. Ajabu |
| 6. | A. Chanda na pete | B. maziwa na tui | C. kinu na mchi | D. shilingi kwa ya pili |
| 7. | A. ulimithili | B. ulimithilika | C.ulimithilia | D. ulimithilishwa |
| 8. | A. ilikuwa | B. ulikuwa | C. ungekuwa | D. unakuwa |
| 9. | A. chake | B. yake | C. yao | D. kwao |
| 10. | A. Kwa sababu | B. Hata hivyo | C. Ijapokuwa | D. Mighairi |

11. A. zilijaa B. kulijaa C. yalijaa D. ilijaa
12. A. jamaa B. jamii C. familia D. kijamii
13. A. Alimrai B. Aliona C. Alijua D. Alimkisia
14. A. yao B. zake C. wake D. yake
15. A. faraga B. kiokosi C. fungule D. nia

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 2. | 3. | 4 | 5 |
| 6. | 7. | 8. | 9. | 10. |
| 11. | 12. | 13. | 14. | 15. |

## MTUNGO 2

Watu ___1___ upungufu au ____2___ wanapaswa kuonewa imani na ___3___ na jamii.Katu, uatilifu ____4____ msingi wa ___5___ mtu yoyote yule. ____6___, inasikitisha kuona kuwa wengi wao ____7____ bila kupewa msaada wowote. Mtu yeyote yule ____8___ na kumdhihaki yule mwenye upungufu kwani ____9____.

1. A. wenye wana B. waliyo na C. wana D. walio na
2. A. walegevu B. walemavu C. walaanifu D. wadhaifu
3. A. kuchukuliwa B. kutunzwa C. kuambaliwa D. kuengwaengwa
4. A. Isiwe B. asiwe C. usiwe D. yasiwe
5. A. Kumpendelea B. kumbagua C. kumpendekeza D. kumtwaza
6. A. Ingawa B. Ilhali C. Mighairi D. Hata hivyo
7. A. wametekelezwa B. wametekelezwa C. wametelekezwa D. wamelegezwa
8. A. asijitwike magago B. asimpige jeki C. asijikweze mbega D. asione gere
9. A. aliyekupa kiti ndiye aliyenipa kumbi B. mpanda ovyo hula ovyo C. mwekaji kisasi haambiwi mwerevu D. bidii ya mja haiondoi kudura

Kuanzia leo utambue kwamba wewe ___10___ uwezo ___11____ kujifunza na kuelewa mambo ____12____ duniani. Wewe ___13___ kama wengine ___14___ kufaulu vizuri sana maishani ___15____.

10. A. hauna B. huna C. una D. haina
11. A. ya B. wa C. za D. la
12. A. mengi B. nyingi C. mingi D. ndiyo
13. A. yu B. u C. m D. ndiyo
14. A. wanaweza B. wameweza C. wanaoweza D. wanayoweza
15. A. mwao B. yao C. zao D. lao

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 2. | 3. | 4 | 5 |
| 6. | 7. | 8. | 9. | 10. |
| 11. | 12. | 13. | 14. | 15. |

## MTUNGO WA 3

***Jaza mapengo yote***

Mara ___1____ kilipolia wachezaji wa pande ___2___ mbili walijitokeza ___3___ wakionekana ___4____ huku ___5___ wanaringaringa. Watu wakawafanya waongeze ____6___ yao kwa kuwashangilia kwa ___7___ za makofi na ___8____. Haukupita ___9____ mrefu walitengana ___10___ sehemu zao na kipenga cha kuanzisha mchezo kikalia. Naam, timu zilianza ___11___ shika, mara ___12___ ukatupwa huku na huko, kila upande ___13___ kupata ushindi lakini ___14___ hizo ziliendelea hadi mwisho. Tulizidi kupiga moyo ___15____.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. firimbi | B. kipenga | C. kipengo | D. kengele |
| **2.** | A. zote | B. yote | C. wote | D. kote |
| **3.** | A. shuleni | B. nyumbani | C. ugani | D. uani |
| **4.** | A. wapambe | B. vichojo | C. watumishi | D. watanashati |
| **5.** | A. wakikuwa | B. wakawa | C. wawe | D. wakiwa |
| **6.** | A. mzaha | B. madoa | C. madaha | D. vipawa |
| **7.** | A. vifijo | B. hoihoi | C. vigelegele | D. hoiyee! |
| **8.** | A. mbija | B. bija | C. mbinja | D. binja |
| **9.** | A. saa | B. munda | C. muda | D. mda |
| **10.** | A. katika | B. kwa | C. kando | D. ndani |
| **11.** | A. vuta | B. kufa | C. pata | D. vita |
| **12.** | A. kandanda | B. mpira | C. kubumbu | D. ngozi |
| **13.** | A. ukishindana | B. ukiwania | C. wakitaka | D. ukionea |
| **14.** | A. mvutano | B. ligi | C. mchuano | D. kukurukakara |
| **15.** | A. ngumi | B. bao | C. ndondi | D. konde |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | **2.** | **3.** | **4** | **5** |
| **6.** | **7.** | **8.** | **9.** | **10.** |
| **11.** | **12.** | **13.** | **14.** | **15.** |

## MTUNGO WA 4

***Jaza mapengo yote***

Mwishoni ___1___ mwezi ____2___ na mawazo ___3___ "Sasa ninaweza ___4____ mahitaji yangu ___5____. Ngoja nianze kutafuta ____6___ kilicho jirani na ___7____ kwangu ili ___8___ ufanisi ____9____ kazini."

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. mwa | B. ya | C. wa | D. na |
| **2.** | A. nilijia | B. nilijiwa | C. nilikujiwa | D. nilijiliwa |
| **3.** | A. jipya | B. mpya | C. mapya | D. mipya |
| **4.** | A. kuinunua | B. kujinunulia | C. kuzinunua | D. kununulia |

5. A. ubinafsi B. binafsi yangu C. kibinafsi D. binafsi
6. A. chumba B. makao C. nyumba D. banda
7. A. nyumba B. kazi C. kazini D. maskani
8. A. niburike B. niboreshe C. niboreke D. niboronge
9. A. langu B. zangu C. yangu D. wangu

Mja ___10___ kwa makosa yake mwenyewe ___11____ kuwa ___12____. Maoni yangu ni kuwa ___13___ nyingine mtu ___14___ madhara bila kujua kwamba anajidhuru. Hivyo, afaa mwongozo wa namna ya kurekebisha. Je, mtu kama huyu ataambiwa maneno ____15____?

10. A. anapotozwa B. anapoteseka C. napotesa D. anapoteza
11. A. hutusiwa B. hushurutishwa C. huambiwa D. huombiwa
12. A. mchimba kisima huingia mwenyewe
    B. mwiba wa kujichoma hauna kilio
    C. heri nusu ya shari kuliko shari kamili
    D. kuteleza si kuanguka
13. A. wakati B. nafasi C. nyakati D. muda
14. A. hujikutisha B. hukuletea C. humletea D. hujikusia
15. A. yayo hayo B. hayo yayo C. iyo hiyo D. hiyo hiyo

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 2. | 3. | 4 | 5 |
| 6. | 7. | 8. | 9. | 10. |
| 11. | 12. | 13. | 14. | 15. |

## SARUFI

***Jibu swali kulingana na maagizo uliyopewa***

1. Chagua sentensi iliyo sahihi.
   A. mbao ya msonobari huwa nzuri kwa ujenzi.
   B. Nywele ikichanwa vizuri hupendeza sana.
   C. Nyembe zenye kutu husababisha pepopunda.
   D. Nyuta za nyumba zimepakwa rangi ya kupendeza.

   1.

2. Chagua ***kivumishi*** cha pekee katika sentensi hii
   ***Tunda lolote gumu halililiki vizuri***
   A. Gumu
   B. Vizuri
   C. Halililiki
   D. Lolote

   2.

3. Ibadili sentensi ifuatayo katika hali ya wingi
   ***Waya wa shaba hupitisha umeme vizuri***
   A. Waya wa shaba hupitisha umeme vizuri
   B. Nyaya ya shaba hupitisha umeme vizuri
   C. Waya ya shaba hupitisha umeme vizuri
   D. Nyaya za shaba hupitisha umeme vizuri

   3.

4. Upi ni udogo wa sentensi ifuatayo?
***Mlima huu ni mrefu kuliko yote***
A. Kilima hiki ni kirefu kuliko kote.
B. Kijilima hiki ni kirefu kuliko yote.
C. Kilima hiki ni kirefu kuliko vyote.
D. Kijilima hiki ni kirefu kuviliko vyote.

5. Sentensi zifuatazo zinaonyesha hali ya kufanyiza ***isipokuwa***
A. Mbegu zilizooza haziwezi kumea.
B. Ni nani aliyemliza mtoto yule?
C. Dawa mujarabu itakuponya upesi.
D. Mtego wangu umemnasa kitwitwi.

6. Rais alipokagua gwaride askari walisimama tisti
***Kielezi ni kipi katika sentensi hii***
A. Walisimama
B. Tisti
C. Wote
D. Gwaride

7. Maelezo yapi hayatatui maana ya neno ***"vua"*** ________________
A. Kuondoa kilichovaliwa mwilini.
B. Kukamata samaki kwa nyavu.
C. Kuondoa makumbi ya nazi.
D. Kumwondoa mtu katika tatizo.

8. Badili katika usemi halisi; Kaka alitaka kujua iwapo ningeenda sokoni siku hiyo
A. Kaka aliniuliza, "Tutaenda sokoni leo"
B. Kaka alinieleza, "Utaenda sokoni leo?"
C. Kaka aliniuliza, "Unaenda sokoni leo?"
D. Kaka aliniuliza, "Utaenda sokoni leo?"

9. Chagua sentensi yenye kihisishi kifaacho zaidi
A. Labeka! Naja sasa hivi!
B. Shabbash! Ni mdudu gani Yule?
C. Ah! Umesema huyu ni baba yako.
D. Yarabi! HUmu mna mtu?

10. Kitenzi kutokana na nomino ***mlafi*** ni ________________
A. Lafi
B. Kula
C. Lifi
D. Lapa

11. Andika katika usemi wa taarifa
***"Nitaenda kuogelea kesho tukiwa na rafiki yangu," Musa alisema***
A. Musa alisema ataenda kuogelea siku iliyofuata akiwa na rafiki yake.
B. Musa alisema angeenda kuogelea kesho akiwa na rafiki yake.
C. Musa alisema ningeenda kuogelea siku iliyofuata nikiwa na rafiki yangu.
D. Musa alisema kuwa angeenda kuogelea siku iliyofuata akiwa na rafiki yake.

| |
|---|
| 4. |
| 5. |
| 6. |
| 7. |
| 8. |
| 9. |
| 10. |
| 11. |

12. Ndovu hutetea naye nyoka ________
A. huhisi
B. huluza
C. huvuma
D. hunguruma

12.

13. Chagua sentensi yenye kielezi kiigizi.
A. Maji yalimwagika mwa!
B. Kazi ili ifanywa ovyo ovyo.
C. Karani na Wafula waliwasi salama salimini.
D. Nembu alijibu maswali kitaalamu.

13.

14. Bainisha matumizi ya "ki"
***Bwana Wabora amemwoa msichana wa kiarabu.***
A. Kivumishi
B. Kiwakilishi
C. Kielezi
D. Masharti

14.

15. Mama wee! toba! Mungu wangu! Ni viingizi vya kuonyesha
A. Wogoa
B. Dharau
C. Majuto
D. Kufurahi

15.

16. Chagua nomino halisi
A. Umati wa watu
B. Jumanne
C. Wema
D. Uyoga

16.

17. Kimilikishi mkato wa baba yako ni ________
A. Babako
B. Babayo
C. Babao
D. Babaako

17.

18. Bainisha matumizi ya "na"
***Nina magari matatu mapya***
A. Kuonyesha kukubaliana
B. Kuonyesha mtendaji
C. Kuonyesha hali ya kumiliki
D. Kuonyesha wakati uliopo

18.

19. Ni nini kinyume cha sentensi hii.
***Mwamu ameuziwa koo na kijana.***
A. Wifi ameuziwa koo na kijana
B. Wifi amenunuliwa pora na mzee
C. Wifi amenunuliwa jogoo na mzee
D. Shangazi amenunuliwa jogoo na mzee

19.

20. Ni sentensi gani yenye kiunganishi cha kulinganisha
A. Umechelewa kwenda shuleni ilhali unajua kuwa utaadhibiwa
B. Watu wote walihudhiria harusi isipokuwa Musa
C. Maembe na machugwa ni matamu
D. Nilinua gunia la mchele sembuse la usufi

20.

21. Nomino mateso na maabara hupatikana katika ngeli gani?
A. I - ZI
B. LI - YA
C. YA - YA
D. U - ZI

21.

**22.** Kati ya jozi hizi ni ipi ambayo haijaandamanishwa vyema na kisawa chake? 22.

A. Ng'ombe - bakari
B. Kitenzi - kiarifa
C. Kiwakilishi- kibadala
D. Gashi - kijulanga

**23.** Naomba kijiko cha ______________ wali. 23.

A. kukula
B. kula
C. kulia
D. kukulia

**24.** Wanafunzi waliingia katika darasa. Neno "*katika*" ni ______________ 24.

A. Kiunganishi
B. Kihusishi
C. Kielezi
D. Kilinganish

**25.** Mvua ______________ masika aghalabu husababisha mafuriko na maafa mengi 25.

A. wa
B. za
C. la
D. vya

## MSAMIATI

**1.** Rumande ni ______________________ 1.

A. wanapowekwa wale kesi zao zinaendelea.
B. wanapowekwa wanaotumikia kifungo.
C. seli ya kufungia washukiwa katika kituo cha polisi.
D. wanapoketi wale wanaosikiliza kesi.

**2.** Mtu anayebeba mizigo huitwa haya yote isipokuwa ______________ 2.

A. kuli
B. hamali
C. mpagazi
D. mchukuzi


**3.** Andazi gumu linalopikwa kwa unga wa mtama ni ______________ 3.

A. mahamri
B. ladu
C. kaimati
D. ngumu

**4.** Ni kiumbe yupi aliyeambatanishwa vizuri na maradhi anayoeneza? 4.

A. Panya - tauni
B. Mbung'o - malaria
C. Nzi - kifaduro
D. Konokono - kisonono

**5.** Sehemu ya mguu inayoonyeshwa kwa kishale huitwa ______________ 5.



A. kisigino
B. muundi
C. nguyu
D. wayo

6. Kati ya jamaa hawa yupi aliyetoka upande wa mama?
   A. Mbiomba
   B. Hau
   C. Mwamu
   D. Amu

7. Gani si msamiati wa mekoni?
   A. Susu
   B. Rafu
   C. Mashizi
   D. Mwiku

8. Wakati ambao jua huzama huitwaje? ____________
   A. Macheo
   B. Alasiri
   C. Machweo
   D. Adhuhuri

9. Mahali ambapo vitu vya kale huwekwa ili kuwa kama kumbukumbu huitwa ____________
   A. ufuo
   B. kumbukumbu
   C. jokofu
   D. makavazi

10. Mahali kwenye nyumba ambapo moshi hutokea huitwaje?
    A. Uchagaa
    B. Utu
    C. Dohani
    D. Mlango

11. Nyama zinazoshikilia meno huitwaje?
    A. Taya
    B. Fisi
    C. Gundi
    D. Fizi

12. Ugonjwa wa kichocho husababishwa na ____________
    A. Mbung'o
    B. Mbu
    C. Nondo
    D. Konokono

13. Malipo ya kuolea mke huitwa ____________
    A. Mahali
    B. Fidia
    C. Mahari
    D. Ridhaa

14. Mtu anayeyatunza maktaba na kuazimisha vitabu ni ____________
    A. Mhandisi
    B. Hatibu
    C. Mmktaba
    D. Mkutubi

15. Mashindano yalianza wakati wa mtikati. Huu ni wakati gani?
    A. Usiku wa manane
    B. Alfajiri
    C. Adhuhuri
    D. Alasiri

16. Kilemba cha jogoo huwa na rangi gani?
    A. Samawati
    B. Nyekundu
    C. Nyeusi
    D. Kijivu

17. Mtu anayebeba mizigo kwa malipo ni ____________
    A. hamali
    B. utingo
    C. mshenga
    D. chura

18. Nywele zilizo kati ya pua na mdomo wa juu katika uso wa mtu ni ____
    A. ndevu
    B. kionjamchuzi
    C. masharubu
    D. malaika

19. Makao ya mchwa ni ____________
    A. makafani
    B. dahalia
    C. kilinge
    D. kichuguu

| |
|---|
| 6. |
| 7. |
| 8. |
| 9. |
| 10. |
| 11. |
| 12. |
| 13. |
| 14. |
| 15. |
| 16. |
| 17. |
| 18. |
| 19. |

**20.** Mke wa mwana ni ____________________ 20.

A. mkazamjomba
B. mwanyumba
C. mkazamwana
D. mkemwenza

**21.** Mama aliniagiza nizidi ______________ ili chakula kiive haraka. 21.

A. kupekecha
B. kupuliza moto
C. kukoka
D. kupasha moto


**22.** Eneo kame ambalo halina nyasi wala miti ila mchanga ni ________ 22.

A. nguu
B. tambarara
C. msitu
D. jangwa

**23.** Kanchiri huvaliwa wapi? 23.

A. Kidarini
B. Kiunoni
C. Kichwani
D. Mikononi

**24.** Mchoro huu unaonyesha ala inayoitwa ________________ 24.



A. Zumari
B. Saksofoni
C. Kinubi
D. Gitaa

**25.** Maradhi ya kushindwa kupumua vizuri ni ______________ 25.

A. Pumu
B. Kifaduro
C. Kiharusi
D. Mafua

## INSHA

*Mahitaji ya uandishi wa Insha*

1. Hati nzuri inayosomeka kwa urahisi.
2. Urefu unaokubalika, yaani isipungue ukurasa 1½.
3. Lugha sanifu isiyokuwa na makosa ya sarufi.
4. Matumizi mazuri ya misamiati inayolenga mada uliyopewa.
5. Matumizi mazuri ya fani mbali mbali ili kupamba lugha K.V. methali, t[illegible], Istiara n.k.
6. Mtiririko mzuri wa mawazo mazito.
7. Sentensi fupi fupi zinazoeleweka kwa urahisi.
8. Ulengaji mada husika.
9. Kutumia mbinu mbali mbali kama taharuki ili kuvuta mawazo ya msomaji.